

# HALMASHAURI YA MJI NZEGA

SHULE YA SEKONDARI MIGUWA,  
S. L. P 213,  
NZEGA.

TAREHE .....

Kumb Na.MSS/F.I. 2021/.....

JINA LA MWANAFUNZI .....  
S. L. P .....

## **YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MIGUWA HALMASHAURI YA MJI NZEGA MKOA WA TABORA MWAKA 2021.**

### **1.0. Utangulizi.**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechagulia kijiunga na kidato cha kwanza katika Shule hii mwaka 2021. Shule hii ya sekondari Miguwa ipo katika kijiji cha Miguwa kata ya Miguwa umbali wa km 15 kutoka Makao makuu ya Halmashauri ya mji wa Nzega.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11/01/2021. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 04/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 15/01/2021 ndani ya wiki mbili (02) tu.

### **2.0. Mambo muhimu ya kuzingatia.**

#### **2.1. Sare za shule**

- a) Sare ya shule hii ni suruali (02) za rangi ya DAMU YA MZEE, Kitambaa kizito, shati (02) nyeupe mikono mifupi, viatu vyeusi vya kamba na soksi nyeusi kwa wavulana. Sketi (02) rangi ya DAMU YA MZEE kitambaa kizito, shati (02) nyeupe mikono mifupi viatu vyeusi vya kamba na soksi nyeupe kwa wasichana. Maelezo ya mshono ni suruali isiwe modo (ya kubana), sketi ya marinda na iwe ndefu kupita magotii.
- b) Rangi ya Hijabu ifanane na sare za shule
- c) Sare ya michezo kwa shule hii ni tisheti rangi ya kijivu zenyenembo ya shule, raba, soksi ndefu za bluu na bukta za bluu (2) kwa wote.

- 2.2. **Vifaa vya taaluma:-** Daftari kaunta book Q3 tisa (9), kalamu za kutosha za wino wa bluu na nyeusi, penseli HB, rula nzito nyeupe na mkebe wa hesabu.

### **3.0. Sheria na kanuni muhimu za shule hii.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na Ofisi ya Raisi – TAMISEMI zenyе jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu nchini.

### **UNATAKIWA KUZINGATIA MAMBO YA MSINGI YAFUATAYO HAPA SHULENI:-**

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za shule ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii
- e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
- f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- h) Kutunza mali za shule.
- i) Uaminifu.
- j) Kutii maagizo halali utakayopewa na uongozi wa shule.
- k) Kuheshimu bendera ya taifa.
- l) Kuwahi shuleni na kutoka kwa muda uliopangwa.
- m) Kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za shule.
- n) Kukamilisha kwa wakati mhitaji yote uliyoagizwa.
- o) Mwanafunzi wa kidato cha kwanza anatakiwa kupanda mti atakao utunza hadi anapomaliza kidato cha nne na ataukabidhi uongozi wa shule.

### **3.2. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule:-**

- a) Wizi
- b) Uasherati na Ushoga
- c) Ubakaji
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyia kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
- e) Kupigana au kupiga
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- g) Kudharau Bendera ya Taifa
- h) Kuwa mijamzito/ kupata mimba
- i) Kuoa/ kuolewa
- j) Kutoa mimba
- k) Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- l) Kukataa adhabu kwa makusudi
- m) Kuwa mtoro
- n) Kuwa na simu ya mkononi.

**4.0. Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.**

- a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na Mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
- c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

**5.0. Tafadhal soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu. Mzazi aje na mwanaye wakati wa kuripoti shuleni.**

**6.0. Kumbuka kumpatia elimu mtoto ni lazima. Hivyo mtoto akishindwa kuripoti kwa wakati hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mzazi/mlezi wa mototo husika.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

.....  
**MWL. LYOBA H. MBOGO  
MKUU WA SHULE  
0786 495 255 / 0757 424 103**